# KOMBE LA SHIRIKISHO | KANUNI

## TOLEO LA 2021



TANZANIA FOOTBALL FEDERATION

TFF

SHIRIKISHO LA MPIRA WA MIGUU TANZANIA

Play Fair Be Positive

www.tff.or.tz

tfftanzania

tanfootball

tanfootball

TFF TV

Tanfootball

Tanfootball

TFF online Radio

TANZANIA FOOTBALL FEDERATION

TFF

SHIRIKISHO LA MPIRA WA MIGUU TANZANIA

**Karume Memorial Stadium/Shaurimoyo Road**

1574, Dar es Salaam - Tanzania

+255 22 2182032, Fax: +255 22 2182031

tanfootball@tff.or.tz

www.tff.or.tz

# YALIYOMO


**I Uchezaji wa Kiungwana**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Uchezaji wa Kiungwana | 9 |

**II Utawala**

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Matumizi na Tafsiri | 18 |
| 3 | Kuundwa | 19 |
| 4 | Mamlaka | 20 |
| 5 | Usimamizi | 21 |
| 6 | Ngao ya Jamii | 23 |
| 7 | Udhamini | 24 |
| 8 | Vyombo vya Maamuzi | 27 |

**III Uendeshaji**

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Shindano | 30 |
| 10 | Msimu na Ratiba | 31 |
| 11 | Uthibitisho wa Kushiriki | 32 |
| 12 | Mfumo | 33 |
| 13 | Fainali ya Kombe la Shirikisho | 34 |
| 14 | Mshindi | 35 |
| 15 | Taratibu za Mchezo | 36 |
| 16 | Uwanja | 37 |
| 17 | Maafisa wa Mchezo | 38 |
| 18 | Tuzo | 39 |

# YALIYOMO


**IV Udhibiti**

19 Adhabu 42

**V Usajili**

20 Usajili 46

**VI Fedha**

21 Mapato na Gharama 49

22 Huduma za Mchezo 51

**Azimio**

Azimio 52


TFF





















## Sura: I UCHEZAJI WA KIUNGWANA (FairPlay)

### 1 Uchezaji wa Kiungwana

(1) Wachezaji wanatakiwa kuzingatia Kanuni KUMI (10) za FIFA za Uchezaji wa Kiungwana wakiwa Ndani na Nje ya Uwanja.

#### 1.1 Cheza Kiungwana

Ushindi hauwezi kuwa na thamani iwapo umepatikana katika njia isiyo halali au kwa udanganyifu. Kudanganya ni rahisi lakini haileti raha ya ushindi. Kucheza kiungwana inahitaji moyo na tabia njema. Pia hufurahisha zaidi. Mchezo wa kiungwana siku zote una malipo yake hata kama utapoteza mchezo. Kucheza kiungwana kunakujengea heshima wakati kudanganya kunaleta aibu. Kumbuka kuwa mpira wa miguu ni mchezo na mchezo wowote hauwezi kuwa na maana kama hautochezwa kiungwana kwa kuzingatia kanuni na taratibu ili mshindi halali aweze kupatikana.

## 1.2 Cheza kutafuta Ushindi, kubali kushindwa

Kushinda ndiyo lengo la kushiriki katika mchezo wowote ule. Siku zote usijiandae kushindwa. Iwapo huchezi kwa nia ya kushinda utakuwa unawadanganya wapinzani wako, unawadhulumu watazamaji na pia unajifanya mwenyewe kuwa ni mjinga. Usikate tamaa hata siku moja unapopambana na wapinzani wenye nguvu zaidi lakini pia usidharau hata siku moja unapopambana na wapinzani dhaifu. Ni kumkosea adabu mpinzani unapocheza chini ya kiwango chako. Cheza kwa nia ya kutafuta ushindi hadi dakika ya mwisho lakini kumbuka hakuna anayeshinda wakati wote. Siku nyingine utashinda na siku nyingine utashindwa. Jifunze kukubali kushindwa. Usitafute visingizio unapofungwa. Sababu za kweli siku zote zitadhihirika. Wapongeze washindi bila kinyongo. Usilaumu waamuzi wala mtu mwingine yoyote. Jizatiti kufanya vizuri zaidi wakati mwingine. Walioshindwa na kukubali wanapata heshima zaidi kuliko washindi wanaolazimisha.

## 1.3 Heshimu Sheria za Soka

Michezo yote inalindwa na sheria. Bila sheria itakuwa ni vurugu tupu. Sheria za mpira wa miguu ni nyepesi na rahisi kujifunza. Hakikisha unajifunza; itakusaidia kuufahamu mpira wa miguu vizuri zaidi. Kuufahamu mchezo zaidi itakufanya uwe mchezaji bora zaidi. Pia ni muhimu kufahamu madhumuni ya sheria zilizowekwa. Zimekusudiwa kuufanya mchezo uwe na ladha katika kuucheza na kuuangalia. Kwa kufuata sheria, mchezo wa mpira wa miguu utakuwa na burudani zaidi.

## 1.4 Heshimu Watu wa Kada zote

Mchezo wa kiungwana unamaanisha kuheshimu wapinzani. Bila ya wapinzani kutakuwa hakuna mchezo. Kila mmoja ana haki sawa, ikiwemo haki ya kuheshimiwa. Wachezaji wa timu moja ni wenza. Tengeneza timu ambayo kila mmoja kwenye timu atakuwa na haki sawa. Waamuzi wapo kuhakikisha nidhamu na mchezo wa kiungwana unadumishwa. Siku zote kubali maamuzi yao bila ya ulalamishi, na wasaidie waweze kuwafanya washiriki wote waufurahie zaidi mchezo. Viongozi pia ni sehemu ya mchezo na wanatakiwa wapewe heshima wanayostahili. Watazamaji wanaufanya mchezo uwe na msisimko. Wanahitaji kuuona mchezo ukichezwa kiungwana kwa kuzingatia kanuni, lakini pia wanatakiwa kuwa waungwana na kujiheshimu.

## 1.5 Dumisha Maslahi ya Mpira wa Miguu

Mpira wa miguu ndiyo mchezo unaoongoza duniani. Lakini siku zote unahitaji msaada wa kila mmoja kuufanya uendelee kuwa mchezo wenye kupendwa zaidi. Fikiria maslahi ya mpira kabla ya maslahi yako mwenyewe. Fikiria ni vipi vitendo vyako vinaweza vikaupaka matope mchezo wa mpira wa miguu. Zungumzia mambo mazuri ya mchezo wa mpira wa miguu. Shawishi watu wengine kuuangalia na kuucheza kiungwana. Wasaidie wengine kupata burudani ya kutosha katika mchezo wa mpira wa miguu kama unayoipata wewe. Kuwa balozi wa mchezo wa mpira.

## 1.6 Waheshimu Wanaolinda Heshima ya Soka

Jina zuri la mchezo wa mpira wa miguu limeendelea kudumu kwa sababu idadi kubwa ya watu wenye kuupenda mchezo huu ni wakweli na waungwana. Wakati mwingine mtu hufanya jambo kubwa ambalo linastahili tulitambue. Watu kama hawa wanastahili kutuzwa na mambo mema waliyofanya yatangazwe. Hii itashawishi wengine kuiga mifano yao. Saidia kuendeleza mpira wa miguu kwa kuyatangaza mazuri yake.

## 1.7 Kataa Mambo Mabaya yota

Umaarufu mkubwa wa mchezo wa mpira wa miguu wakati mwingine huufanya uwe rahisi kuathiriwa na mambo mabaya ya nje. Jichunge na vishawishi vitakavyokufanya ushawishike kushiriki kwenye kudanganya au kutumia madawa yaliyokatazwa. Madawa yaliyokatazwa hayana nafasi katika soka, mchezo mwingine wowote na jamii kwa jumla. Sema hapana kwa madawa ya kulevya. Saidia kuupiga teke ubaguzi kwenye soka. Wachukulie wachezaji wote na wengineo kuwa ni sawa bila kujali dini zao, kabila, jinsia au utaifa wao. Usivumilie hata kidogo kamari katika michezo unayoshiriki. Inaporomosha kiwango chako cha uchezaji na inasababisha hali ya mgongano wa maslahi. Thibitisha kuwa soka haihitaji fujo, hata kutoka kwa washabiki wako wenyewe. Soka ni mchezo na michezo huleta amani.

## 1.8 Wasaidie Wengine Kupambana na Rushwa

Wakati mwingine unaweza kusikia wachezaji wenzako au watu wengine unaowafahamu wanashawishiwa wadanganye kwa njia moja au nyingine au washiriki katika vitendo visivyokubalika katika mchezo wa soka. Wanahitaji msaada wako. Usisite kusimama upande wao. Wape nguvu ya kukataa vishawishi. Wakumbushe wajibu wao kwa wenzao na kwa mchezo wenyewe. Tengeneza umoja wenye mshikamano, kama ngome ngumu kabisa kwenye mchezo wa soka.

## 1.9 Wabainishe Wanaouchafua Mchezo wetu.

Usione aibu kusimama dhidi ya yoyote yule ambaye una hakika anashawishi wengine kudanganya au kushiriki katika vitendo vingine visivyokubalika. Ni vyema kuwafichua waovu wote ili waweze kuondolewa kabla ya kuleta madhara. Ni uovu kushirikiana na watu waovu. Usiseme tu hapana, wafichue wanaotaka kuichafua soka kabla hawajafanikiwa kuwashawishi wengine.

## 1.10 Tumia Soka Kujenga Dunia Bora Zaidi.

Soka ina nguvu ya ajabu ambayo inaweza kutumika kuifanya dunia kuwa sehemu bora zaidi ya kuishi. Tumia nguvu hii kudumisha amani, usawa, afya na elimu kwa wote. Ifanye soka iwe bora zaidi, ipeleke kwa jamii kujenga dunia bora zaidi.

(2) Pamoja na Mazingatio ya Utekelezaji Kanuni 1.1.1 – 1.1.10 Wachezaji pia Wanawajibika Kuzingatia na kudumisha kwa ukamilifu wake Kanuni 1.2.1 – 1.2.10 wakati wote wawapo kiwanjani.

(2.1) Kudumisha tabia njema nje ya uwanja na wakati wote wa mchezo kwa kucheza bila ya kuwaumiza au kuhatarisha usalama wa wachezaji wa timu pinzani.

(2.2) Kutodanganya kuumia au kufanyiwa rafu, kutotumia mbinu chafu mchezoni au kutotukana kwa maneno, ishara au kujihusisha na vitendo vyovyote vya kibaguzi.

(2.3) Kutorejeshea (retaliation) iwapo utafanyiwa rafu au kukashifiwa.

(2.4) Ni nahodha pekee ambaye anaruhusiwa kuzungumza na waamuzi. Iwapo patatokea malamiko yoyote wakati wa mchezo wachezaji wengine wote wanatakiwa wawe hatua zisizopungua kumi kutoka kwa mwamuzi.

(2.5) Mchezaji wakati wote anatakiwa atii maagizo ya kocha wake. Mchezaji anatakiwa akubali kubadilishwa uwanjani na kuadhibiwa kutokana na vitendo vya utovu wa nidhamu au visivyokuwa vya kiuanamichezo.

(2.6) Mchezaji anatakiwa amheshimu na atii maagizo ya nahodha wake nje na ndani ya uwanja hususan katika masuala yahusuyo timu na tabia njema kwa jumla.

(2.7) Mchezaji anatakiwa awaheshimu wachezaji wenzake na awatie hamasa nje na ndani ya uwanja. Mchezaji anatakiwa asimkashifu mchezaji mwenzake mwenye kufanya makosa.

(2.8) Mchezaji anatakiwa awape wachezaji wa timu pinzani heshima yao, awe tayari kutoa msaada kwa mchezaji aliyeumia na kushikana mikono kabla na baada ya mchezo.

(2.9) Mchezaji anatakiwa wakati wote kuheshimu maamuzi ya waamuzi na kutozozana nao au kutumia lugha ya matusi au kashfa dhidi yao.

(2.10) Mchezaji anatakiwa ajiheshimu mwenyewe na ajitunze na asitumie madawa yaliyokatazwa



# SURA YA PILI
# UTAWALA

# Sura: II UTAWALA

## 2 Matumizi na Tafsiri

Katika Kanuni hizi isipokuwa pale ambapo imeainishwa vinginevyo itatafsiriwa na kumaanisha kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **TFF** | **Tanzania Football Federation**<br>Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania |
| **FIFA** | **Federation Internationale de Football Associations**<br>Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Mpira wa Miguu |
| **CAF** | **Confederation of African Football**<br>Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika |
| **FA(M)** | **Regional Football Association**<br>Chama cha Mpira cha Mkoa |
| **KAMATI ya UTENDAJI** | Kamati ya Utendaji wa TFF |
| **LIGI** | Ligi husika kilabu inayoshiriki |
| **KILABU** | Kilabu cha timu inayoshiriki Kombe la Shirikisho |
| **TIMU** | Timu inayoshiriki Kombe la Shirikisho |
| **KILABU MSHINDI** | Kilabu Bingwa wa Kombe la Shirikisho |
| **MPIRA** | Mpira wa kuchezea |
| **LIGI KUU** | Ligi Kuu ya Tanzania Bara |

## 3 Kuundwa

Kanuni hizi zimeundwa chini ya Ibara ya 75 (3) ya Katiba ya TFF ya mwaka 2020 na zitatumika Tanzania Bara.

## 4 Mamlaka

(1) Kwa minajili ya kufafanua kanuni hizi TFF itakuwa inatoa WARAKA maalum kila inapoonekana inafaa kufanya hivyo kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Kanuni hizi.

(2) Kamati ya Utendaji ya TFF inaweza kurekebisha kanuni hizi kila inapotokea haja na sababu za msingi za kufanya hivyo, aidha TFF itatoa WARAKA maalum utakaosomeka pamoja na Kanuni hizi kwa marekebisho yoyote yaliyofanyika ambayo hayajaingizwa katika kitabu cha kanuni hizi. Kamati ya Utendaji ya TFF ndio chombo pekee chenye Mamlaka ya Kutafsiri au/na kufuta Kanuni hizi.

(3) Mambo kadhaa yasiyosomeka moja kwa moja humu yametolewa maelekezo ya kusomeka kwenye kanuni za Ligi husika, halikadhalika mambo mengine yasiyokuwemo kwenye Kanuni hizi yataamuliwa na Kamati husika au ya Utendaji ya TFF kwa kuzingatia Kanuni za TFF, FIFA na CAF na kwa mujibu wa katiba ya TFF.

## 5 Usimamizi

(1) Kombe la Shirikisho litasimamiwa na kuendeshwa na Kamati ya Mashindano ya TFF kwa mujibu wa kanuni hizi. Kamati ya Mashindano itawajibika kushirikiana na vyombo vingine vya TFF katika masuala yaliyo katika mamlaka ya vyombo hivyo.

(2) TFF inaweza kushughulikia/kufanyia uchunguzi na kufanyia uamuzi kwa mujibu wa Kanuni hizi, au Kanuni nyingine za adhabu za TFF, CAF na FIFA jambo lolote lisilo la kawaida, la hatari au lisilo la kiuanamichezo lililotokea katika mchezo wa Kombe la Shirikisho au katika mwenendo wa shughuli za Kombe la Shirikisho.

(3) TFF inaweza kusimamisha kwa kipindi maalum au muda usiojulikana matumizi ya Kituo chochote au Uwanja wowote kwa michezo ya Kombe la Shirikisho au Mashindano yote ya TFF endapo itabainika katika Kituo/Uwanja husika kukithiri vitendo vya fujo na vurugu au kuthibitika kwa mazingira ya kutopatikana haki kwa timu yoyote na kutoheshimika au kutendewa visivyo maafisa wa mchezo.

(4) Kamati ya Mashindano inaweza kufuta adhabu ya kadi yoyote iliyotolewa uwanjani na mwamuzi na kuondoa adhabu inayoambatana na kadi hiyo endapo inathibitika bila mashaka kuwa mtuhumiwa hakustahili kadi hiyo.

(5) Kamati ya Mashindano itakutana katika hali ya kawaida kwa ratiba ya vikao itakayoratibiwa na Sekretarieti ya TFF kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Kamati. Aidha Kamati itakutana kwa dharura ndani ya saa 72 (sabini na mbili) wakati wowote linapojitokeza jambo la dharura au la kushughulikiwa kwa haraka kuhusiana na uendeshaji na usimamizi wa Kombe la Shirikisho.

(6) Kamati ya Mashindano ya TFF itachukua hatua moja kwa moja kwa vitendo vyovyote vya uvunjifu wa Kanuni vilivyo na ushahidi usio na mashaka vilivyotokea katika michezo ya Kombe la Shirikisho la TFF au kuhusiana moja kwa moja na mchezo ya Kombe la Shirikisho la TFF bila ya kujali mahitaji ya kupelekwa kwenye vyombo vingine vya TFF.

(7) Kamati ya Mashindano ya TFF itashiriki katika Usimamizi na Uendeshaji wa Michezo ya Kombe la Shirikisho moja kwa moja vituoni kwa Utaratibu utakaopangwa na Sekretariet ya TFF na katika mazingira ya uwepo wa Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti wa Kamati, atakuwa ndio Msimamizi Mkuu kwa mchezo husika.

(8) Makamishna na Wasimamizi wengine wa Michezo kwenye michezo ya Kombe la Shirikisho watateuliwa/kusimamia kutokana na nafasi zao katika Mashindano mengine ya TFF na Ligi husika za Timu shiriki kwenye Kombe la Shirikisho kwa Mazingatio ya Hadhi kwa Daraja la Juu miongoni mwa Madaraja ya timu husika zinazoshindana.

(9) Katika Mazingira maalum ya Majanga kiasi cha kusababisha Kombe la Shirikisho kushindwa kuendelea kwa muda unaoathiri Kalenda ya msimu katika hali ya kutorekebishika TFF itafuta Shindano hilo kwa msimu husika na Hali itasalia kama ilivyomalizika Msimu uliotangulia.

(10) Kombe la Shirikisho katika Ngazi ya Mkoa (na wilaya zake) litasimamiwa na Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa husika ambapo, FA (M) itaendesha Shindano kwa Mazingatio ya Kalenda na Muongozo wa Kombe la Shirikisho uliotolewa na TFF. Vyombo vya Maamuzi kwa Mkoa husika vitashughulikia masuala yote kwenye Kombe la Shirikisho kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## 6 Ngao ya Jamii

Kilabu Bingwa wa Kombe la Shirikisho itashiriki kwenye Mchezo wa Ngao ya Jamii katika Ufunguzi wa Msimu unaofuata kwa kupambana na Kilabu Bingwa wa Ligi Kuu. Masharti na Taratibu zote za Mchezo wa Ngao ya Jamii ni kama inavyosomeka kwenye vipengele vya Kanuni ya Ngao ya Jamii ya Kanuni za Ligi Kuu ya Tanzania Bara.

## 7 Udhamini

(1) Mdhamini wa Kombe la Shirikisho anaweza kutajwa kwenye jina la Shindano kukidhi mahitaji ya Mkataba. Timu zote shiriki zinawajibika kufuata maelekezo ya mahitaji ya mkataba wa Udhamini kwenye maeneo yao.

(2) Nembo ya mdhamini itawekwa kwa rangi zake halisi kwenye mkono wa jezi upande wa kulia katika mazingira ya mdhamini kutoa jezi hizo au vilabu kutumia jezi zao. Timu na maafisa wa mchezo watawajibika kutumia jezi/vifaa vilivyo na nembo husika.

(3) TFF Itatoa Muongozo na Maelekezo kuhusu Masharti na Makubaliano ya Msingi ya Mkataba ambapo Kilabu, Waamuzi na Wachezaji watawajibika kufuata katika michezo yote ya Kombe la Shirikisho.

(4) Timu zinazoshiriki Kombe la Shirikisho na waamuzi wanatakiwa wahakikishe wanavaa vifaa vilivyotolewa na Mdhamini wa Kombe la Shirikisho (endapo vimetolewa) katika michezo na shughuli za Kombe la Shirikisho.

(5) Timu zitalazimika kuweka nembo ya mdhamini kwenye vifaa vyake vya kuchezea kama inavyoelekezwa na Kanuni hizi au kwa Maelekezo Maalum ya TFF.

(6) Kilabu zote zitakuwana haki sawa ya nafasi ya matangazo ya wadhamini wake wa kilabu kwenye michezo yote ya Kombe la Shirikisho bila ya kujali timu mwenyeji na mgeni. Mabango Yasiozidi nane katika vipimo vya 600cm x 90cm kwa kila bango kwa kila timu.

(7) Matangazo yasiyokuwa ya wadhamini Kombe la Shirikisho au klabu au yasiyoidhinishwa na TFF hayatoruhusiwa kwenye maeneo ya uwanja wakati wa michezo na shughuli zinazohusiana na Kombe la Shirikisho

(8) Kilabu inawajibika kuheshimu masharti ya udhamini wa Kombe la Shirikisho kimkataba kwenye michezo yake kama inavyoelekezwa na TFF, timu itakayokiuka itatozwa faini ya shilingi milioni tatu (3,000,000/-) kwa kila mchezo itakaokiuka na inaweza kuchukuliwa hatua zaidi ikiwemo kufungiwa

(9) Kilabu itakayofanya jambo lolote (ambalo halihusiani na mchezo wake) la kukiuka masharti ya mikataba ya wadhamini kama ilivyoelekezwa na TFF itatozwa faini ya shilingi milioni tatu (3,000,000/-) na endapo itakaidi zaidi inaweza kuchukuliwa hatua zaidi ikiwemo kuondolewa kwenye Kombe la Shirikisho.

(10) Timu haitaruhusiwa kuvaa au kutumia nembo au kuweka tangazo la kibiashara lililo na ushindani wa moja kwa moja na bidhaa ya/za mdhamini zinazotambulika katika udhamini wa Kombe la Shirikisho.

(11) Pande zote shiriki katika Kombe la Shirikisho zinawajibika kuheshimu na kuzingatia masharti ya mkataba wowote wa udhamini na ukiukwaji wowote utavutia uwekwaji wa vikwazo na adhabu kutolewa na TFF.

(12) Klabu haziruhusiwi kufanya mawasilaino ya moja kwa moja na Mdhamini kwa jambo lolote bila usimamizi wa TFF, ukikuwaji wowowte utavutia vikwazo na adhabu

(13) Haki zote za matangazo kwenye viwanja inapochezwa michezo ya Kombe la Shirikisho ni mali ya TFF. TFF itaweka mazingatio kwa matangazo ya Wadhamini wa Kombe la Shirikisho pamoja na Wadhamini binafsi wa kilabu waliotambuliwa na TFF.

(14) Masharti mengine yanayotokana na Mikataba ya Udhamini yatakuwa kama yanavyosomeka kwenye Kanuni za Ligi kwa timu husika.

## 8 Vyombo vya Maamuzi

(1) Malalamiko yoyote na Pingamizi kwa Mchezo na Mchezaji yatafuata Utaratibu kwa mujibu wa Kanuni za Ligi kwa timu husika iliyo na mahitaji husika.

(2) Vyombo vya Maamuzi vitashughulikia Malalamiko yoyote kwa mujibu wa Utaratibu wa Kanuni kwa mazingatio ya Kanuni na Viwango vya Adhabu kwa timu inayolalamikiwa.

(3) Wakati wowote katika mazingira ya Mapungufu ya Kikanuni kwa Kanuni kuhusiana na mojawapo ya Ligi miongoni mwa timu zinahusika na shauri husika, Kanuni za Ligi Kuu zitatumika.

(4) Taratibu mbalimbali za Udhibiti na Miongozo itasomeka kama ilivyoainishwa ipasavyo kwenye Kanuni za Ligi za timu husika. Wahusika wanawajibika kufuata Kanuni za Ligi kwa Miongozo ya Uendeshaji, Udhibiti na Adhabu.


2020 - 2021
KCB
BANK
SPORTPESA.CO

# SURA YA TATU

# UENDESHAJI

## Sura: III UENDESHAJI

### 9 Shindano

(1) Shindano hili litajulikana kama Kombe la Shirikisho la TFF (TFF Federation Cup) na linaweza kutajwa kwa jina la Mdhamini wa Shindano kwa mazingatio na mahitaji ya kimkataba.

(2) Timu zinazoshiriki Kombe la Shirikisho zitatambuliwa kwa madaraja ziliopo katika Ligi zao husika ambapo taratibu zote za Uendeshaji na Masharti mbalimbali kuhusiana na timu, wachezaji, makocha, Kilabu, maafisa wa mchezo, Usimamizi na viwango na taratibu za Adhabu yatazingatia Kanuni za Ligi husika kwa timu husika na ligi hiyo kuendana na Daraja timu husika ilipo.

(3) Pale palipo na Mapungufu kwenye kanuni za madaraja mengine, Kanuni za Ligi Kuu zitatumika. Vyombo vya Maamuzi vitakuwa na maamuzi kuhusu taratibu mbalimbali na viwango vya adhabu katika mazingira ya aina hii na mengine.

## 10 Msimu na Ratiba

(1) Kuanza kwa Kombe la Shirikisho kutatangazwa na TFF kwa mazingatio ya Kalenda ya Matukio yake kwa kutoa waraka utakaoainisha masuala muhimu kwa msimu husika na kwa mazingatio ya kanuni hizi na kanuni nyingine za TFF.

(2) Ratiba ya Kombe la Shirikisho itafanyika kwa mfumo wa Kubahatisha (Draw) tokea hatua za awali ambayo itaainisha timu inayocheza nyumbani na timu zinazocheza kwa mtindo wa kubahatisha kwa mujibu wa Utaratibu utakaowekwa kukidhi hitajio hilo kwa ufanisi Zaidi

(3) Timu Washindi wa FA Mikoa watathibitisha Ushiriki wao kwa kuambatanisha Usajili wa Wachezaji wa timu husika walioidhinishwa na Chama cha Mpira wa Miguu cha Mkoa husika Pamoja na Hati ya Usajili wa Kilabu ya Msajili wa Vilabu na Vyama vya Michezo nchini.

## 11 Uthibitisho wa Ushiriki

(1) Timu zote za Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi ya Mabingwa wa Mikoa Pamoja na Washindi wa FA kwa kila Mkoa kwa Msimu husika kama zilivyotajwa pia kwenye Kanuni hizi zinawajibika kushiriki Kombe la Shirikisho bila kukosa wala hiyari.

(2) Kombe la Shirikisho lina Mahusiano ya moja kwa moja na Kilabu zote tajwa shiriki kupitia Ligi/Mashindano husika ya Kilabu na hivyo kushindwa kushiriki mchezo mmoja wa Kombe la Shirikisho kwa namna yoyote ile Timu husika inapoteza Hadhi ya kushiriki Ligi ya Daraja iliyopo pamoja na adhabu zinazoambatana nazo kwa mujibu wa Kanuni ya 31 ya Ligi KUU na Kanuni hizo hizo kwenye Ligi ya Madaraja mengine.

(3) Timu itakayoshindwa kushiriki au itakayojitoa kinyume na Utaratibu wa TFF itakabiliwa na adhabu za kufungiwa kwa kipindi kisichopungua miaka miwili Pamoja na adhabu nyingine kwa mujibu wa Kanuni.

(4) Timu itatambulisha Taarifa zake muhimu mbalimbali kama zitakavyohitajika na TFF kupitia Muongozo wa Kombe la Shirikisho utakaotolewa kwa kila Msimu.

## 12 Mfumo

(1) Kombe la Shirikisho litachezwa kwa mfumo wa mtoano kuanzia hatua ya awali mpaka nusu fainali ambapo Fainali itatoa Bingwa na Mshindi wa Pili.

(2) Hatua ya awali timu zitapangwa kutoana kwa lengo la kuleta uwiano wa mtoano kutegemea idadi ya timu zinazotarajiwa kushiriki hatua ya kwanza kwa mazingatio na matarajio ya kupata mtiririko wa mtoano mpaka hatua ya nusu fainali.

(3) Timu zilizoshuka daraja kutoka daraja la pili au jingine na kupata hadhi ya kushiriki Ligi ya Mkoa hazitakuwa na Hadhi ya timu za Ligi ya Mabingwa wa Mikoa ambapo timu zilizopanda daraja kutoka Ligi ya Mbingwa wa Mikoa zitatambulika kama timu za Ligi Daraja la Pili kwa msimu husika.

(4) Mzunguko wa Kwanza utashirikisha timu Mabingwa wa FA Mikoa na timu za Ligi ya Mabingwa wa Mikoa ambapo Washindi na timu za Ligi Daraja la Pili zitaungana tena kwenye Mzunguko wa Pili kwa lengo la kupata timu zitakazotengeneza uwiano kusudiwa wa idadi itakayotimiza timu sitini na nne (64) za Mzunguko wa Pili.

(5) Mzunguko wa Tatu utashirikisha timu sitini na nne (64) ambazo zitakuwa ni timu thelathini na mbili (32) zilizopata ushindi kwenye Mzunguko wa Kwanza, Timu Kumi na Sita (16) za Ligi Daraja la Kwanza na Timu kumi na sita (16) za Ligi Kuu.

(6) Timu zitazopata ushindi kwa kila hatua/Mzunguko zitashiriki Mzunguko unaofuata wa Kombe la Shirikisho.

## 13 Fainali ya Kombe la Shirikisho

(1) Fainali ya Kombe la Shirikisho itachezwa kwenye Uwanja Utakaoteuliwa na TFF Mapema na Maalum kwa ajili hiyo. TFF pia itateua viwanja katika Mikoa tofauti kwa ajili ya Michezo ya Nusu fainali ya Kombe la Shirikisho kwa Msimu husika.

(2) FA (M) husika wa Uwanja wa Fainali au/na Nusu Fainali wa Kombe la Shirikisho itawajibika kuhakikisha Inatimiza Masharti yote na Vigezo vilivyowekwa kwa Mujibu wa Muongozo wa fainali ya Kombe la Shirikisho.

(3) Timu shiriki wa Fainali (finalists) zinatakiwa kufika Kituo cha Fainali sio chini ya masaa arobaini na nane (48hrs) kabla ya mchezo wa Fainali.

(4) Timu Shiriki za Mchezo wa Fainali (finalists) zitawajibika kushiriki Programu zote kama zinavyoelekezwa kwenye Muongozo wa Fainali ya Kombe la Shirikisho.

(5) TFF inaweza kubadili Uwanja wa Fainali au/na wa Nusu Fainali ya Kombe la Shirikisho endapo Mkoa husika wa Uwanja ulioteuliwa awali umeshindwa kutimiza masharti ya msingi kwa mujibu wa Muongozo wa Fainali ya Kombe la Shirikisho baada ya kujiridhisha kutokana na matokeo ya Ukaguzi uliofanyika.

## 14 Mshindi

(6) Katika mchezo wowote wa Kombe la Shirikisho, mshindi itakuwa ni timu iliyofunga goli/magoli mengi zaidi ya timu pinzani katika mchezo baina yao.

(7) Katika Hatua nyingine za Kombe la Shirikisho Endapo timu zitalingana kwa idadi ya goli/magoli katika mchezo baina yao (zitatoka sare) hakutakuwa na muda wa nyongeza, mchezo huo utaamuliwa kwa timu kupigiana mikwaju ya penati kwa mujibu wa sheria za penati baada ya dakika tisini za mchezo kumalizika.

(8) Kwa Michezo ya Hatua ya Nusu Fainali na Fainali Mshindi atapatikana kwa mchezo kuongezwa Dakika thelathini za nyongeza (Extra Time) endapo timu Mshindi hatapatikana kwenye Dakika tisini za kawaida za Mchezo ambapo Utaratibu wa Sheria ya Penati Utatumika endapo Mshindi pia atakosekana baada ya muda wa nyongeza (Extra Time).

(9) Mshindi wa Mchezo wa Fainali wa Kombe la Shirikisho atatambuliwa kama Kilabu Bingwa ya Kombe la Shirikisho kwa msimu husika na atazawadiwa Kikombe cha Ubingwa na stahiki nyingine kwa mujibu wa Utaratibu.

(10) Bingwa wa Kombe la Shirikisho ataiwakilisha Tanzania kwenye Mashindano ya Kombe la Shirikisho la Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika CAF (CAF Confederation Cup - CCC).

(11) Mshindi yoyote wa Kombe la Shirikisho atakayeteuliwa na TFF kushiriki Mashindano yoyote kutokana na hadhi ya nafasi yake kwenye Kombe la Shirikisho atawajibika kucheza.

## 15 Taratibu za Mchezo

(1) Michezo yote ya Kombe la Shirikisho itachezwa kwa kufuata sheria kumi na saba (17) za mpira wa miguu za FIFA (FIFA 17 laws of the game).

(2) Taratibu za Mchezo kwenye Michezo ya Kombe la Shirikisho itakuwa kama zinavyosomeka kwenye kanuni za Ligi husika kwa kila timu.

(3) Viwango vya Adhabu vinavyotokana na ukiukwaji wa Taratibu za Mchezo vitakuwa kama vinavyosomeka kwenye Kanuni za Ligi kwa timu husika.

## 16 Uwanja

(1) Uwanja wowote Utakaotumika kwa michezo ya Kombe la Shirikisho ni lazima Uthibitishwe na TFF kwa mujibu wa Vigezo vilivyowekwa. TFF inaweza kubadilisha uwanja wowote kwa mchezo wa Kombe la Shirikisho endapo itathibitika mazingira ya mashaka makubwa ya kiusalama au hali isiyorekebishika kwa mazingatio ya masharti katika Leseni za Kilabu katika muda hitajika kwa mahusiano na mchezo husika.

(2) Uwanja wa Nyumbani wa Kilabu yoyote kwa Kombe la Shirikisho Utatambuliwa kama ulivyotambulishwa na Timu husika kwa Michezo yake ya nyumbani kwa mujibu wa Kanuni katika Ligi ya Daraja Kilabu husika inayoshiriki.

(3) Katika mazingira maalum, Kilabu ya Daraja la chini au kwenye Hatua za awali za Kombe la Shirikisho, kilabu inaweza kuomba kwa TFF juu ya matumizi ya uwanja mwingine tofauti na uwanja wake au wa Mkoani mwake endapo kuna sababu za msingi au dharura. Maamuzi ya TFF katika hali hii yatakuwa ya mwisho.

(4) Kilabu haitakuwa na Ruhusa ya Uchaguzi wa Uwanja mwingine kwa Michezo yake ya Nyumbani kama ilivyotolewa kwenye kanuni 9.7 ya Kanuni za Ligi Kuu.

(5) TFF itateua Mapema Viwanja kwa Michezo ya Nusu Fainali na Fainali ya Kombe la Shirikisho kwa kila Msimu.

(6) TFF ina mamlaka ya mwisho ya kuhamisha mchezo katika uwanja mwingine au kubadilisha kituo cha mchezo kwa sababu inazoona zinafaa kwa mchezo na wakati husika.

## 17 Maafisa wa Mchezo

(1) Maafisa wa Mchezo kwa Mchezo wa Kombe la Shirikisho watatokana na Maafisa waendeshaji na wasimamizi katika Ligi za daraja tofauti ambapo uteuzi kwa kila mchezo wa Kombe la Shirikisho Utazingatia Hadhi kwa mchezo husika ambapo Darala la Timu iliyo katika Daraja la Juu zaidi kwa kila mchezo itakuwa ndio Hadhi husika ya mchezo na Maafisa wa Mchezo watapangwa kwa Mazingatio ya Hadhi husika.

(2) Utaratibu kuhusu Waamuzi wa Kombe la Shirikisho utakuwa ule ule kama ilivyo kwa Mashindano yote ambapo Kamati ya Waamuzi kwa kushirikiana na Sekretariet ya TFF itahusika kwa teuzi za Waamuzi wa Kombe la Shirikisho na kwa mazingatio ya kanuni ya 17.1 ya kanuni hizi.

## 18 Tuzo

(1) Timu Bingwa wa Kombe la Shirikisho itatunukiwa kikombe cha ubingwa kwenye Mchezo wa Fainali ya Kombe la Shirikisho. Mshindi wa Pili atatunukiwa zawadi zitazoandaliwa kwa ajili yake.

(2) Kilabu kitahodhi Kombe la Shirikisho kilichoshinda mpaka hapo kitapotakiwa kukirejesha na TFF. Endapo kilabu kitafanikiwa kuchukua Kombe la Shirikisho mara tatu mfululizo kitalitwaa kombe hilo moja kwa moja.

(3) Kutakuwa na mchezaji Bora wa kila Mchezo wa Kombe la Shirikisho kuanzia hatua ya Robo Fainali atakayeteuliwa na kuzawadiwa baada ya kila mchezo kumalizika.

(4) Medali, tuzo na kikombe kingine chochote kinachotolewa kama zawadi kwenye shughuli za Ushiriki wa Kombe la Shirikisho havitarejeshwa, vitakuwa vya kudumu kwa aliyetunukiwa.

(5) Washindi wa vikombe na Tuzo mbalimbali katika Kombe la Shirikisho watapatikana kwa mujibu wa Kanuni hizi na kanuni za Ligi ya timu husika na Vigezo vya Tuzo vitakavyowekwa na TFF na kupitia kwenye Mchakato kwa mujibu wa TFF na kutolewa kwenye Sherehe ya Tuzo za TFF kwa kila Msimu.


WINNERS
2020 - 2021

## SURA YA NNE

# UDHIBITI

## Sura: IV UDHIBITI

### 19 Adhabu

(1) Masuala yote ya kinidhamu na udhibiti wa makosa mbalimbali yanayohusu timu, kilabu, mchezaji, kocha, kiongozi wa kilabu na ufundi, waamuzi, makamishna na watendaji na mwingine yoyote kuhusiana na Kombe la Shirikisho yatashughulikiwa kwa mujibu wa Kanuni za Ligi husika kwa timu husika na katika kanuni zilizo na masharti maalum itazingatiwa daraja la kilabu husika katika utoaji wa adhabu na udhibiti wa mienendo.

(2) Pale palipo na Mapungufu kwenye kanuni za madaraja mengine, Kanuni za Ligi Kuu zitatumika. Vyombo vya Maamuzi vitakuwa na maamuzi kuhusu viwango vya adhabu katika mazingira ya aina hii na mengine.

(3) Adhabu za kufungiwa kunakotajwa muda kwa muhusika yoyote zitamfanya muhusika kuwa katika zuio la kushiriki shughuli za Mpira wa Miguu/michezo ya Mashindano ya TFF kwa ujumla wake na si tu kwa Kombe la Shirikisho au Ligi ya timu husika bila ya kujali adhabu ilitolewa kwenye shidano gani.

(4) Adhabu za Malipo ya Faini zinaweza kushughulikiwa kwa muhusika au kilabu yake kukatwa fedha kwenye stahili zake zozote zinazosimamiwa na TFF endapo yatakuwepo mazingira ya ucheleweshwaji wa malipo au kukosekana kwa nia au uwezo wa kulipa.

(5) Adhabu za Kadi za njano na nyekundu zinazotokana na michezo ya Kombe la Shirikisho zitahesabiwa kwa pamoja na kadi zinazopatikana kwenye Ligi ya Timu husika na mchezaji/kiongozi wa ufundi anawajibika kutumikia adhabu husika kwa mujibu wa kanuni.

(6) Adhabu za kusimamishwa idadi ya michezo kwa mchezaji zinahusisha Mashindano yote ya TFF yanayohusu kilabu husika.

(7) Mchezaji ambaye bado anatumikia adhabu ya kadi nyekundu aliyoipata katika ushiriki wake kwenye kilabu yake kwa msimu husika ataendelea kutumikia adhabu husika kwenye msimu unaofuata au katika msimu huohuo endapo atakuwa amehamia kilabu nyingine.


SportPesa
amtv

# SURA YA TANO
# USAJILI

## Sura: V USAJILI

### 20 Usajili

(1) Wachezaji wanaoshiriki Kombe la Shirikisho ni wachezaji waliosajiliwa rasmi na vilabu husika shiriki kwa mujibu wa Ligi za TFF na ni wachezaji waliothibitishwa tu usajili wao na kupewa leseni za kuchezea kwa msimu husika na kwa mujibu wa Kanuni za Ligi husika ndio wanaoruhusiwa kuwakilisha timu zao kwenye mchezo wowote wa Kombe la Shirikisho.

(3) Majina ya mchezaji yanawajibika kujazwa yote matatu kama yalivyoandikishwa kwenye usajili wake wakati wowote kwenye mahitaji ya kujaza jina la mchezaji.

(4) Wachezaji wa timu za Vijana na wachezaji wa Kigeni wanaoruhusiwa kushiriki mchezo wowote wa Kombe la Shirikisho watafanya hivyo kwa mazingatio ya Kanuni za Ligi.

(5) Viongozi wa Ufundi wa Timu husika waliondikishwa na kusajiliwa kwa ajili ya Timu kwenye Ligi ya Timu husika ndio hao hao wataendelea kuwa Viongozi wa Ufundi kwa Timu husika kwenye kombe la Shirikisho na kwa Mazingatio ya Masharti yote maalum kwa Viongozi wa Ufundi wa timu kwa mujibu wa Kanuni za Ligi husika.

(6) Adhabu zozote zinazotokana na ukiukwaji wa taratibu za mchezo zinazohusisha usajili zitatambulika kama inavyosomeka kwenye Kanuni za Adhabu kuhusiana na hadhi ya mchezaji na hukumu zake kwa mazingatio ya makosa ya kiusajili yanayobatilisha matokeo ya mchezo na yasiyo.


WINNERS
ASFC
TFF
AZAM SPORTS FEDERATION CUP
FIFA

# SURA YA SITA
# FEDHA

## Sura: VI FEDHA

### 21 Mapato na Gharama

(1) Mgawanyo wa Mapato ya Mchezo (*gate collection*) utafanywa kwa kutumia Fomu ya Mapato ya TFF maalum kwa matumizi hayo kwa mazingatio ya viwango vya asilimia husika kwa kila eneo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

| | | |
|---|---|---|
| | Jumla ya PATO | |
| 1.1 | VAT | **18%** |
| | Baki ya PATO | |
| 1.2 | BMT | **3%** |
| 1.3 | Gharama za Tiketi (kiwango husika) | |
| | Baki ya PATO | |
| 1.4 | Timu Mwenyeji | **25%** |
| 1.5 | Timu Mgeni | **25%** |
| 1.6 | Mamlaka ya Uwanja | **15%** |
| 1.7 | TFF | **19%** |
| 1.8 | Gharama za Mchezo | **10%** |
| 1.9 | FA (M) | **6%** |

(2) Msimamizi wa Kituo anawajibika kusimamia shughuli zote zinazohusisha Mapato na Gharama Pamoja na mgawanyo kwa wahusika wote stahiki na atawasilisha taarifa ya mapato na fedha za mchezo husika kwa TFF katika muda usiozidi masaa arobaini na nane (*48hrs*). Kiongozi au Msimamizi atakayeshindwa kuwasilisha atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Kanuni za TFF.

(3) Malipo na Stahili mbalimbali kuhusiana na Kombe la Shirikisho ni kama inavyoelekezwa kwenye Muongozo wa Kombe la Shirikisho kwa Msimu husika na kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za TFF.

## 22 Huduma za Mchezo

(1) Huduma ya Kwanza, Tiba, Bima na Gari la Wagonjwa kwa mchezo husika zitakuwa kwa Mazingatio ya Masharti kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Ligi husika ya timu shiriki.

(2) Huduma nyingine za Mchezo kama Ulinzi na Usalama, Matayarisho ya Kiwanja (Pitch), Vijana wa Mipira (Ball Kids), Ubao wa kubadilishia wachezaji (Substitution Board), MCM, Matangazo Uwanjani (Public Address System), Itifaki ya VVIP (Protocol), Utaratibu wa Tiketi na Uingiaji Uwanjani Pamoja na Huduma kwa Wanahabari, Viwanja vya Mzoezi kwa timu vitakuwa ni Jukumu la Msimamizi wa Kituo na FA (M) husika.

## AZIMIO

Kanuni hizi zimepitishwa kwa Azimio la Kamati ya Utendaji ya TFF iliyokutana Dar es Salaam tarehe 14 Agosti 2021

TANZANIA FOOTBALL FEDERATION
TFF
SHIRIKISHO LA MPIRA WA MIGUU TANZANIA

**Wallace KARIA**
Rais

**Wilfred KIDAO**
Katibu Mkuu


Kigoma
kfa
ciation


Fair, Be

www.tff.or.tz

tfftanzania

tanfootball

tanfootball

TFF TV

Tanfootball

Tanfootball

TFF online Radio


SHIRIKISHO LA MPIRA WA MIGUU TANZANIA

**Karume Memorial Stadium/Shaurimoyo Road**

1574, Dar es Salaam - Tanzania

+255 22 2182032, Fax: +255 22 2182031

tanfootball@tff.or.tz

www.tff.or.tz

**Play Fair**
Be Positive

TANZANIA FOOTBALL FEDERATION

TFF
SHIRIKISHO LA MPIRA
WA MIGUU TANZANIA